GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVIII Nam. 6785 **6 Novemba, 2019** **Bei Shs. 2,500/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Mawakili Sura ya 28 na Sheria ya Wakuu wa Viapo Sura ya 29 na kutunga Sheria ya Mawakili na mambo mengine yanayohusiana na hayo 272

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Mawakili Zanzibar, 2019

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 27 Novemba, 2019 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
6 Novemba, 2019

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matanagazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanayoweza kutiwa katika Gazeti. Nakala ya matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinuduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa
SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAWAKILI SURA YA 28 NA SHERIA YA WAKUU WA VIAPO SURA YA 29 NA KUTUNGA SHERIA YA MAWAKILI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mawakili Zanzibar, 2019 na itaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika kwa Mawakili,mavakili na Wakuu wa viapo wote Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakili" maana yake ni mtu aliyesajiliwa na kukubaliwa kuwa Wakili chini ya masharti ya Sheria hii;

"Baraza la Mawakili" maana yake ni Baraza lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Baraza la Sheria au mtu yeyote anayekaimu nafasi hiyo;

"mtaka huduma" inajumuisha mtu yeyote ambaye, kama ni muhusika Mkuu au kwa niaba ya mwengine, au akiwa kama mdhamini au muwakilishi, au kwa nafasi yoyote, ana uwezo wa kupewa kwa maandishi au kutokana na hali halisi iliyopo, kuzuwia au kuajiri au kukaribia kushikilia au kuajiri wakili au vakili au mtu yeyote ambaye anawajibika kulipa gharama kwa wakili au vakili;

"Gharama" inajumuisha ada,tozo, malipo, matumizi na mishahara;

"Kazi yenye majadiliano" inajumuisha kazi yoyote inayofanywa na Wakili au Vakil Mahakamani katika shauri au mwenendo wowote wa kisheria;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu ya Zanzibar na mahakama nyenginezo zilizo chini ya mahakam kuu;

"Waraka" maana yake ni waraka wowote unaohusiana na mwenendo wa kisheria au waraka wowote unaotumika kuanzisha, kubainisha, kutoa dhamana ,kuweka mipaka au kutafautisha haki yoyote, umiliki au maslahi ikiwa kwa kupewa kukusudiwa kupewa kuhusiana na mali isiyohamishika mbali na Wasia;

(a) Waraka unaohusiana na mali isiyohamishika ulioandaliwa katika mfumo wa maandishi katika mfumo unaostahiki kama unavyoainishwa katika Miongozo ya Usajili wa Nyaraka;

(b) Waraka unaohusiana na mali isiyohamishika ambao usajili wake ni wa hiari chini ya Sheria za usajili wa Nyaraka au Sheria nyengine inayotumika;

"Mitihani" maana yake ni mitihani ya kisheria inayoandaliwa na Baraza la Mawakili chini ya Sheria hii;

"Wakili wa kigeni" maana yake ni mtu ambaye amepewa mamlaka au amesajiliwa kufanya kazi za Sheria katika nchi yoyote isiyokuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Mfuko wa Mahakama" maana yake ni Mfuko ulioanzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama;

"Huduma za kisheria" maana yake ni huduma ambazo wakili au vakil anaweza kisheria kuzitoa chini ya Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria;

"Kazi isiyo na majadiliano" inajumuisha kazi yoyote inayohusiana na kuuza, kununua kukodisha, kuweka rehani, kufikia mapatano na mambo mengine ya uhaulishaji;

"Mkuu wa Kiapo" maana yake ni Wakili anayefanya kazi za uwakili na amethibitishwa na Jaji mkuu kuwa Mkuu wa Viapo;

"Cheti cha kukubaliwa kufanya kazi za Uwakili" maana yake ni cheti kinachotolewa na Mrajis chini ya kifungu cha 26 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahakama Kuu na itakapohitajika itajumuisha Naibu Mrajis;

"Afisa Kodi" maana yake ni Mrajis au Afisa yeyote anayeteuliwa na Jaji Mkuu kwa uteuzi maalum au wa jumla kwa madhumuni ya kusimamia kodi;

"Vakil" maana yake ni mtu yeyote aliyethibitishwa na Jaji Mkuu kufanya kazi za kisheria akiwa ni Vakil kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa na Jaji Mkuu.

SEHEMU YA PILI
BARAZA LA MAWAKILI

Kuanzishwa na muundo wa Baraza la Mawakili.

4.-(1) Kunaanzishwa Baraza la Mawakili ambalo litakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Jaji wa Mahakama Kuu atakaeteuliwa na Jaji Mkuu ambae atakuwa ni Mwenyekiti;

(b) Mwanasheria Mkuu au muwakilishi wake;

(c) Mkurugenzi wa Mashtaka au muwakilishi wake;

(d) Mkuu wa Skuli ya Sheria ya Zanzibar au muwakilishi wake;

(e) Rais wa Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar au muwakilishi wake;

(2) Mrajis atakuwa Katibu wa Baraza la Mawakili.

Muda wa mwenyekiti kushikilia nafasi yake.

5.-(1) Mwenyekiti wa Baraza atashikilia nafasi yake kwa kipindi cha miaka mitatu lakini anaweza kuteuliwa tena.

Kazi za Baraza la Mawakili.

6. Baraza la Mawakili litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuweka viwango vya kitaalamu kiutendaji na maadili kwa mawakili na vakil;

(b) kuwafanyisha mitihani watu wanaokusudia kuingia katika kada ya Sheria Zanzibar;

(c) kupendekeza kwa Jaji Mkuu majina ya watu wanaotaka kuthibitishwa kuwa wakili na vakil;

(d) kushirikiana na Skuli ya Sheria ya Zanzibar, au Jumuiya ya wanasheria wa Zanzibar, kufanya Semina na kuandaa mijadala katika mada za kisheria itakayoandaliwa na wataalamu wa sheria waliobobea; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote kwa mujibu wa Sheria hii.

Uwezo wa Baraza la Mawakili.

7. Baraza la Mawakili litakuwa na uwezo wa kufanya yafuatayo:

(a) Kusimamia kanuni za mawakili na vakil zinazohusiana na utendaji wa kazi zao kisheria na kitaalamu

(b) Kuunda kamati; na

(c) Kufanya jambo lolote litakalopewa kwa mujibu wa Sheria hii au sheria nyengine zilizopo.

Ukomo wa nafasi ya mwenyekiti.

8. Mwenyekiti atasita kuwa mwenyekiti:

(a) Kwa kumalizika muda;

(b) Kuondolewa na Mamlaka iliyomteuwa;

(c) Kujiuzulu; au

(d) Kufariki.

Uwezo wa Baraza la Mawakili. kukasimu.

9.-(1) kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Baraza la Mawakili linaweza kukasimu utekelezaji wa kazi yoyote kwa kamati yoyote itakayoanzishwa na Baraza la Mawakili.

(2) Baraza la Mawakili linaweza kutekeleza kazi yoyote ya Baraza la Mawakili chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki bila ya kujali utekelezaji wa kazi hiyo kwa kamati iliyokasimiwa.

Vikao vya Baraza la Mawakili.

10. Baraza la Mawakili litafanya vikao vyake mara moja kila baada ya miezi mitatu na linaweza kukutana wakati wowote itakapohitajika.

Akidi.

11.-(1) Wajumbe wanne waliohudhuria kikao wanaweza kukamilisha akidi.

(2) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Baraza la Mawakili ambavyo anahudhuria, na akiwa Mwenyekiti hayupo katika kikao, wajumbe waliohudhuria watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao.

(3) Maamuzi yote ya vikao vya Baraza la Mawakili yatafanywa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria.

(4) Wakati wa vikao mwenyekiti atakuwa na kura ya kawaida na endapo ikitokea hali ya usawa wa kura, mwenyekiti atakuwa na kura ya veto.

Utaratibu wa kuendesha vikao.

12. Baraza la Mawakili linaweza kujiwekea utaratibu wa kuendesha vikao vyake na hasa kuhusiana na namna ya kupanga vikao, taarifa za vikao, uendeshaji wa vikao, utunzaji wa kumbukumbu za vikao, uhifadhi, na uandaaji na ukaguzi wa kumbukumbu.

Matumizi ya Baraza la Mawakili.

13. Fedha za matumizi yatakayofanywa na Baraza la Mawakili katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii zitapatikana kutoka mfuko wa Mahakama.

SEHEMU YA TATU
KUKUBALIWA NA KUSAJILIWA KUWA WAKILI AU VAKIL

Maombi ya kukubaliwa kuwa Wakili.

14.-(1) Mtu anaweza kupeleka maombi kwa jaji mkuu ya kukubaliwa kujiunga kuwa Wakili ikiwa mtu huyo ana sifa zifuatazo:

(a) Shahada ya Kwanza ya Sheria kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) Stashahada ya uzamili katika fani ya Sheria kutoka Skuli ya Sheria ya Zanzibar au inayolingana nayo yenye kutambulika na Baraza la Mawakili; na

(c) Sifa nyenginezo kama itakavyoelezwa na Baraza la Mawakili.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu ambae amekuwa akifanya shughuli za kisheria kama wakili Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi au nchi nyengine kwa kipindi kisichopungua miaka mitano katika nchi ambazo zilitawaliwa na Waingereza, anaweza kuomba kwa Jaji Mkuu kukubaliwa kuwa Wakili Zanzibar.

(3) Mtu asiyekuwa Wakili Tazania Bara, pamoja na masharti yaliyomo katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki atalazimika kupata mafunzo kwa muda usiozidi miezi mitatu, kama itakavyoelezwa na Baraza la Mawakilikwa madhumuni ya kujiweka sambamba na utaratibu wa kufanya shughuli za Kisheria katika Zanzibar.

Maombi ya kukubaliwa kuwa Vakil.

15.-(1) Mtu anaweza kupeleka maombi kwa Jaji Mkuu ya kukubaliwa kujiunga kuwa Vakili ikiwa mtu huyo:

(a) ana Diploma ya Sheria kutoka katika Chuo Kikuu au chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) amepata mafunzo maalum yanayohusiana na mambo ya kisheria si chini ya miezi mitatu Skuli ya Sheria ya Zanzibar au inayolingana nayo yenye kutambulika na Baraza la Mawakili; na

(c) sifa nyenginezo kama zitakavyoelezwa na Jaji Mkuu.

Maombi ya ruhusa kwa Wakili wa kigeni kusimamia kesi.

16.-(1) Wakili wa kigeni ambaye hajasajiliwa Zanzibar ambaye ametokea au anakusudia kuja Zanzibar kwa ajili ya kushiriki katika kesi kama Wakili, anaweza kupeleka maombi ya ruhusa kwa Jaji Mkuu aweze kushiriki katika kesi hiyo.

(2) Wakili aliyeelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, katika maombi yake analazimika kuwasilisha jina la Wakili wa Mahakama Kuu ambaye atakuwa pamoja nae katika kesi hiyo.

(3) Katika sehemu hii “kesi “inajumuisha ombi la ufafanuzi; rufaa, utekelezaji wa hukumu na taratibu za utekelezaji wa hukumu zinazohusiana na shauri.

Jaji Mkuu kuhamishia maombi kwa Baraza la Sheria.

17. Jaji Mkuu analazimika baada ya kupokea maombi ya kukubaliwa chini ya kifungu cha 14 na 15 cha Sheria hii, kuyapeleka maombi Baraza la Mawakilikwa kupata mapendekezo.

Mitihani.

18.-(1) Baraza la Mawakili linalazimika, baada ya kupokea maombi yaliyoelezwa katika kifungu cha 16 cha Sheria hii, kumfanyisha mtihani mtu anaetaka kuruhusiwa kuwa Wakili au vakil.

(2) Baraza la Mawakili linalazimika, iwapo limeridhika kwamba mtu anaetaka kuruhusiwa kuwa Wakili au vakil ametimiza masharti chini ya kifungu cha 14 au 15 cha Sheria hii, na amepata elimu ya kutosha na uzoefu katika fani ya kufanya kazi za kisheria Zanzibar, kumpendekeza mtu huyo kwa Jaji Mkuu aruhusiwe kuwa Wakili au vakil.

Kuruhusiwa kuwa Wakili au Vakili.

19.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 14 na 15 cha Sheria hii, Jaji Mkuu anaweza baada ya:

(a) kupokea mapendekezo kutoka Baraza la Mawakili; na

(b) kutolewa maelezo kuhusu muhusika kama itakavyohitajika, kumruhusu mtu huyo kuwa Wakili au vakili.

Ruhusa inayotolewa kwa Wakili wa kigeni.

20.-(1) Jaji Mkuu anaweza, iwapo ameridhika kwamba wakili anaekusudia kushiriki katika kesi kama wakili ametimiza masharti chini ya kifungu cha 16(1)na (2) cha Sheria hii, kumruhusu kushiriki katika kesi hiyo.

(2) Jaji Mkuu anaweza kutengua ruhusa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki , ikiwa zipo sababu za msingi za kufanya hivyo.

Orodha.

21.-(1) Mrajis atalazimika kutunza orodha ya Mawakili katika orodha tafauti na orodha ya mavakil walioruhusiwa kufanya kazi za kisheria ikiwa sambamba na tarehe zao za kukubaliwa.

(2) Jina, na tarehe ya kukubaliwa kwa mtu aliyekubaliwa, litaingizwa kwa mujibu wa orodha ya utaratibu wa kukubaliwa kwake.

(3) Mtu aliyeruhusiwa kuwa Wakili au Vakil atalazimika kulipa ada iliyowekwa, na Mrajis atalazimika kumpatia mtu huyo Hati ya kukubaliwa iliotiwa saini na Jaji Mkuu.

(4) Jaji Mkuu, iwapo wakati wowote baada ya mtu yeyote kuruhusiwa kuwa Wakili, atabaini kuwa:

(a) maombi, kiapo, cheti au waraka uliopelekwa na mtu huyo, ndani yake yamo melezo ya msingi ambayo ni ya uongo au ya udanganyifu wa hali ya juu, au

(b) cheti kimepatikana kwa njia ya kughushi au udanganyifu: atalazimika kulifuta jina la mtu huyo katika orodha.

Jukumu la Mrajis.

22. Mrajis atatunza maelezo yanayohusiana na mawakili na mavakil walioorodheshwa kama ambavyo itaelezwa, na kufanya mabadiliko stahili kama ambavyo itaonekana inafaa kutokana na sababu ya mabadiliko ya jina au maelezo mengine ya mawakili na mavakil walioorodheshwa chini ya Sheria hii.

Haki za wakili na vakili.

23. Mtu aliyekubaliwa na kuwemo katika orodha ya walioruhusiwa kufanya kazi za kisheria kama wakili na vakili chini ya Sheria hii, kwa kuzingatia mamlaka aliyoruhusiwa kufanya kazi zake hizo na kupata cheti halali, atakuwa na haki ya kufanya kazi hizo za kisheria isipokuwa pale ambapo;

(a) jina lake limefutwa au kuondolewa katika orodha; au

(b) amesitishwa kufanya kazi hizo za kisheria kwa amri ya Mahakama.

Mamlaka ya kufanya kazi za kisheria.

24.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote, mtu asiyekuwa Wakil au vakil ni marufuku kwa mtu huyo, ikiwa ni kwa kutegemea kupata ada, sehemu ya kipato au ziada au tunzo:

(a) Kuwepo mbele ya mahakama au katika bodi, baraza la ushauri au taasisi inayolingana na hizo ambazo wakili au Vakil pekee ndio wanaostahiki kuwepo; au

(b) kuandaa au kuifanyia kazi Hati yoyote au Waraka unaohusiana au unaotakiwa au unaokusudiwa kutumiwa katika kitendo chochote, shauri la madai au mwenedo wa jinai katika mahakama yoyote.

(2) Mtu ambaye si Wakili au Vakili ni marufuku kwake kujifanya kuwa ni mtu wa aina hiyo au kuonesha hali yoyote au kutoa maelezo yanayoashiria au kuonesha wazi kuwa yeye ni wakili au vakil.

(3) Kwa madhumuni ya hapa hakuna kitu chochote ambacho kitaathiri haki ambayo iko wazi kuhusiana na:

(a) Mtu yoyote ambaye majukumu yake yanampasa mtu huyo kutokana na majukumu hayo kuwepo na kukiri mahakamani kwa niaba ya Serikali;

(b) Mdhamini wa serikali, mtu aliepewa jukumu rasmi au mtu yeyote kwa niaba kuwepo mbele ya mahakama chini ya sheria yoyote inayohusiana na ofisi yake;

(c) Mjumbe yeyote wa utumishi wa umma, vyombo vya kisheria, vyombo vinavyojitegemea, au jumuiya za kiraia kuandaa au kutengeneza au kuandaa Hati yoyote au waraka katika kutekeleza jukumu hilo;

(d) Mtu yeyote aliyepewa kazi ya kutoa nakala, kuikamilisha nyaraka au kutafsiri Hati yoyote au waraka; na

(e) mdhamini yeyote au mtu aliyepewa jukumu chini ya sheria zinazohusiana na ufilisi au, mtendaji, au msimamizi, mtunza mali, mfilisi, mfatiliaji ufilisi ambaye ameandaa na kutayarisha hati au warakawowote katika kutekeleza wajibu kisheria na kupokea ada kwa ajili hiyo kama ambavyo inaruhusiwa kisheria.

(4) Mtu yeyote atayevunja masharti ya kifungu hiki ametenda kosa, na atakapotiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania milioni moja au kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita au vyote viwili.

Kuondoshwa.

25.-(1) Wakili au Vakili yeyote aliyekubaliwa anaweza kupeleka maombi kwa Jaji Mkuu jina lake liondoshwe kutoka katika orodha.

(2) Jaji Mkuu anaweza, iwapo ameridhika, akalikubali ombi na kumuelekeza Mrajis kuliondoa jina la muombaji kutoka katika orodha.

SEHEMU YA NNE
CHETI CHA RUHUSA YA KUFANYA KAZI

Cheti cha ruhusa ya kufanya kazi.

26.-(1) Kutakuwa na cheti cha ruhusa ya kufanya kazi kitakachotolewa na mrajis kinachoruhusu mtu kufanya kazi kama Wakili au Vakili.

(2) Wakili au Vakili analazimika kupeleka maombi kwa Mrajis ya kupata cheti cha ruhusa ya kufanya kazi katika mfumo na utaratibu utakaoelezwa katika Miongozo.

(3) Mrajis atalazimika, iwapo ameridhika, na baada ya kupokea malipo ya ada kama itakavyowekwa, kutoa cheti cha kufanya kazi kwa Wakili au Vakili.

(4) Wakili au Vakili atalazimika kuchukua cheti cha kufanya kazi kwa kila mwaka na kulipia ada iliyowekwa.

(5) Cheti cha kufanya kazi kitaweza kutumika kutoka siku kitakapotolewa hadi kufikia tarehe 31 Disemba ya mwaka ambao kimetolewa.

(6) Itakapotokea cheti cha kufanyia kazi kilichotolewa chini ya kifungu hiki kupotea, kuharibika au kuchafuka, kitabadilishwa kwa cheti kingine kipya kufuatia maombi yatakayopelekwa na Wakili au Vakil anayehusika kwa Mrajis na kulipa ada iliyoainishwa katika miongozo.

Kukataliwa cheti cha kufanya kazi.

27.-(1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 26 cha Sheria hii, mrajis anaweza kukataa kutoa cheti cha kufanya kazi kwa wakili au vakil ambaye katika tarehe ya kupeleka maombi ya cheti:

(a) hajaondolewa katika amri ya ufilisi inayoendelea dhidi yake.

(b) umeshatoka uamuzi kuwa yeye ana matatizo ya akili Chini ya Sheria inayohusiana na afya ya akili;

(c) hajalipa fidia yoyote iliyopasa kulipwa dhidi ya muombaji chini ya Sheria hii

(d) hajalipa ada inayostahiki kulipwa; au

(e) ametiwa hatiani kwa kosa la ukiukaji wa maadili

(2) Bila ya kujali kitu chochote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa muombaji atahusika na yaliyoelezwa chini ya aya ya (e) Mrajis anaweza, ikiwa muombaji huyo amepata msamaha usio na masharti, kumpatia cheti hicho.

(3) Katika kifungu sehemu hii neno "ukiukaji wa maadili" linajumuisha udanganyifu na kukosa uaminifu.

(4) Wakili au vakil yeyote ambaye hakuridhika na uwamuzi wa Mrajis kukataa kutoa cheti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa Jaji Mkuu.

Hesabu za mtaka huduma.

28.-(1) Wakili au Vakili atalazimika kufungua na kuweka hesabu benki kwa wataka huduma, na hesabu nyengine kwa ajili yake binafsi.

(2) Jaji Mkuu anaweza kuweka miongozo inayohusiana na hesabu za Benki chini ya kifungu hiki.

(3) Miongozo iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) inaweza kueleza utaratibu ambao utatumiwa katika Afisi za Sheria.

(4) Hatua za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa dhidi ya mtu yeyote atakayekwenda kinyume na muongozo wowote uliowekwa chini ya kifungu hiki.

SEHEMU YA TANO
MALIPO ANAYOLIPWA WAKILI AU VAKIL

Kuanzishwa kwa Kamati ya Ushauri wa Malipo.

29. Kwa madhumuni ya sehemu hii, kutakuwa na kamati itakayojulikana kama Kamati ya Ushauri wa Malipo itakayojumuisha wajumbe wafuatao:

(a) Mrajis wa Mahakama Kuu kama mwenyekiti.

(b) Mkurugenzi anayehusika na Msaada wa Sheria.

(c) Angalau wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka afisi ya Mwanasheria Mkuu; na

(d) Mawakili watatu watakaochaguliwa na Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar.

Kazi za Kamati ya Ushauri wa Malipo.

30.-(1) Kamati ya Ushauri wa Malipo itatoa mapendekezo kwa Jaji Mkuu utaratibu na kipimo cha malipo kwa Wakili au Vakili.

(2) Katika kutoa mapendekezo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kamati ya ushauri wa malipo itazingatia Kazi yenye majadiliano na kazi isiyo ya majadiliano.

(3) Kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake chini ya kifungu hiki, kamati ya ushauri wa malipo itakutana katika mahala na wakati ambao mwenyekiti wa kamati ya ushauri wa malipo ataelekeza.

Matumizi ya kamati ya ushauri wa malipo.

31. Matumizi ya kamati ya ushauri wa malipo katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii zitatolewa kutoka katika mfuko wa Mahakama.

Miongozo ya malipo na kutangaza.

32.-(1) Jaji Mkuu anaweza, baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa kamati ya ushauri wa malipo kuweka Miongozo ya malipo kwa Mawakili na Mavakili.

(2) Jaji Mkuu analazimika kuitangaza miongozo itakayowekwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifuhgu hiki katika Gazeti la Serikali.

Dhamana kutoka kwa mtaka huduma katika kumlipa Wakili au Vakili.

33.-(1) Wakili au Vakili, anaweza kwa kuhusiana na kazi yenye majadiliano na kazi isiyo ya majadiliano kuchukua dhamana kwa mtaka huduma kwa kiwango ambacho atastahiki kupata kama ni mshahara au malipo kwa huduma atakayotoa na faida,

(2) Faida iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki haitatolewa hadi pale ambapo kiwango kinachostahiki kimeshahakikishwa kwa makubaliano au ulipaji kodi.

(3) Kwa mdhumuni ya kifungu hiki, kiwango hicho cha mshahara na malipo kitachukuliwa kuwa kimetolewa kwa mujibu wa makubaliano ,isipokuwa pale ambapo ndani ya mwezi mmoja kuanzia siku lilipotolewa ombi la malipo , mtaka huduma atalalamika au kumtaka Wakili alipie.

(4) Jaji Mkuu anaweza kuweka miongozo itakayoainisha kiwango cha faida kinachostahiki kutozwa katika gharama.

Kufariki, kukosa uwezo au kubadi-lisha, Wakili au Vakili.

34.-(1) Iwapo baada ya huduma kufanywa katika hali ya makubaliano kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria hii lakini kabla ya Wakili au vakil hajakamilisha kazi yake amefariki au amekosa uwezo wa kufanya kazi hiyo, yeyote kati ya wahusika wa pande hizo mbili au muwakilishi wa upande wa yeyote kati yao katika makubaliano anaweza kuomba mahakamani amri ya kuhakikishwa malipo stahiki.

(2) Mahakama inaweza, bila ya kujali kwamba inaona kuwa makubaliano yaliyofanywa hatika hali zote ni ya haki na yenye kukubalika, kutoa amri ya kiwango kinachostahiki kulingana na kazi iliyofanywa ambayo iko mbele yake, inayohakikisha kiwango stahiki, na katika hali hiyo:

(a) afisa anayetoza kodi, katika kuhakikisha kiwango hicho atazingatiwa walichokubaliana katika makubaliano yaliyofanywa, na

(b) kiwango cha malipo atakachokiona kuwa ni stahiki kinaweza kufanyiwa kazi katika utaratibu ambao kama kwamba makubaliano yametekelezwa kikamilifu.

(3) Masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) yatatumika pale tu ambapo mtaka huduma atakapobadilisha Wakili au Vakili kabla ya kukamilika muamala husika.

Ukomo wa kuendeleza Shauri.

35. Kwa kuzingatia Masharti yaliyomo katika Sheria ya ukomo wa muda au Sheria yoyote inayotumika, Mahakama italazimika, iwapo hapana makubaliano ya moja kwa moja katika wakati ambao gharama zilistahiki kulipwa kutupilia mbali kila kesi ya Wakili au Vakili kwa gharama za kesi hiyo au muamala husika uliofanyika.

(a) baada ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia siku Kuanzia tarehe lilipositishwa shauri hilo muamala; au

(b) kuanzia tarehe ambapo Wakili au vakil amesitisha kwa utaratibu muafaka shauri au muamala huo.

SEHEMU YA SITA
WAKUU WA VIAPO

Kukubaliwa kwa wakuu wa viapo.

36. Jaji Mkuu anaweza, baada ya kupokea maombi na malipo ya ada yaliyoainishwa katika miongozo kumkubali Wakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar mwenye uzoefu usiopungua miaka mitano kuwa mkuu wa viapo.

Kuingizwa katika orodha na kupewa cheti mkuu wa viapo.

37.-(1) Wakili anayefanya kazi za kisheria alieainishwa katika kifungu cha 36 cha Sheria hii analazimika ikiwa, Jaji Mkuu ameridhika kwamba ni sahihi kukubaliwa kufanya kazi za Mkuu wa Viapo Zanzibar, na amelipa ada iliyoelezwa katika miongozo na kutia saini orodha iliyowekwa kwa msajili atapewa cheti kuwa mkuu wa viapo kwa utaratibu ulioelezwa katika miongozo.

(2) Wakili anayefanya kazi za kisheria analazimika kila mwaka kuchukua cheti cha mkuu wa viapo na kulipa malipo stahiki.

(3) Cheti cha Mkuu wa Viapo kitatumika kuanzia tarehe kilipotolewa hadi kufikia tarehe 31 Disemba ya mwaka ambao kimetolewa.

(4) Utoaji wa kila cheti cha Mkuu wa kiapo chini ya kifungu hiki utawekwa kumbukumbu kwenye orodha ya wakuu wa viapo.

(5) Itakapotokea cheti cha Mkuu wa kiapo kilichotolewa chini ya kifungu hiki kupotea, kuharibika au kuchafuka, kitabadilishwa kwa cheti kingine kipya kufuatia maombi yatakayopelekwa na mkuu wa viapo anayehusika kwa mrajis na kulipa ada iliyoainishwa katika miongozo.

Adhabu kwa kufanya kazi kinyume na sheria.

38. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 40 cha Sheria hii mtu atakayejifanya kuwa ni Mkuu wa viapo au kupokea ada yoyote au tozo kama mkuu wa viapo bila ya kuwa na cheti cha mkuu wa viapo kilichotolewa chini ya Sheria hii na kinachoendelea kutumika, atakuwa ni mkosa chini ya sheria hii na atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Moja na kwa kosa la mara ya pili au kutiwa hatiani kwa mara nyengine atalipa faini isiyozidi Milioni Mbili au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili.

Katika ithibati ya kiapo kuainishwa pahala na tarehe.

39. Mkuu wa kiapo ambae kiapo kimeapiwa mbele yake chini ya Sheria hii, analazimika kuainisha ukweli katika ithibati ya kiapo ni pahala gani na ni wakati gani kiapo cha hati hiyo ya kiapo kimefanyika.

Jaji au Hakimu wa Mkoa kuwa na baadhi ya uwezo wa Mkuu wa viapo.

40.-(1) Jaji au hakimu wa mkoa kwa nafasi yake kiofisi atakua na uwezo na jukumu la mkuu wa kiapo na atafanya kazi kama mkuu wa viapo katika mambo yafuatayo:

(a) kutoa indhari ya uharamia baharini;

(b) kuzingatia mambo ya upingaji / uzuiaji ya baharini;

(c) kusimamia viapo;

(d) kuthibitisha hati za viapo;

(e) kuthibitisha saini; na

(f) kuthibitisha vivuli vya nyaraka.

(2) Malipo yatakayolipwa kwa kazi za mkuu wa viapo chini ya kifungu hichi itakua ni sehemu ya mapato ya Serikali.

SEHEMU YA SABA
MAADILI NA NIDHAMU ZA MAWAKILI NA MAVAKILI

Kamati ya maadili na nidhamu.

41.-(1) Inaanzishwa kamati itakayojulikana kama kamati ya maadili na nidhamu ambayo inajumuisha wajumbe wafuatao;

(a) Jaji au Jaji mstaafu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama ya Rufaa atakaechaguliwa na Jaji Mkuu;

(b) Mwanasheria Mkuu;

(c) Mkurugenzi wa Mashtaka; na

(d) Raisi wa Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar.

(2) Jaji wa Mahakama Kuu au Jaji mstaafu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama ya Rufaa atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Nidhamu na atakapokuwa hayupo Mwanasheria Mkuu ataongoza vikao.

(3) Ikiwa utendaji wa Raisi wa Chama Cha Wanasheria ndio unaohusiana na malalamiko mbele ya kamati ya maadili na nidhamu, Raisi wa Jumuiya ya Wanasheria ataondolewa katika kikao cha kamati ya maadili na badala yake Jaji Mkuu ataitaka Jumuiya ya Wanasheria kuteuwa mjumbe wa muda ambaye ni Wakili wa Mahakama Kuu Zanzibar.

(4) Kamati ya maadili na nidhamu itateua afisa muandamizi wa umma kuwa ni katibu wa kamati ya maadili na nidhamu.

Vikao vya kamati ya maadili na nidhamu.

42.-(1) Vikao vya kamati ya maadili na nidhamu vitafanyika katika wakati na mahala kama itakavyoamuliwa na mwenyekiti.

Akidi.

43.-(1) Akidi itakua ni wingi wa wajumbe waliohudhuria katika mkutano.

(2) Maamuzi yote yatakayofanywa katika kikao yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria.

(3) Mwenyekiti wa kamati ya maadili na nidhamu katika mkutano atakua na kura ya kawaida na endapo idadi ya kura za wajumbe zitalingana atakuwa atakua na kura maamuzi.

Taratibu za kikao.

44. Kamati ya Maadili na Nidhamu inaweza kuweka taratibu za kuendesha vikao vyake.

Matumizi yatakayofanywa na kamati ya maadili na nidhamu.

45. Matumizi yatakayofanywa na kamati ya maadili na nidhamu katika utekelezaji wa kazi zake chini ya sheria hii yatatoka katika mfuko wa mahakama.

Kubakiza uwezo wa Mahakama katika hatua za kinidhamu.

46. Hakuna kitu chochote katika sehemu hii ambacho kitakiuka, kupunguza, au kitaingilia kati mamlaka yoyote ya mahakama ya kisheria au vyenginevyo katika kushuhulikia jambo lolote linalohusu uvunjaji wa maadili kitaaluma au kosa jengine dhidi ya wakili au vakili alilolifanya wakati wa, katika kuendelea au linalohusiana na mwenendo wowote wa shauri mbele ya mahakama.

Malalamiko dhidi ya Wakili au Vakili.

47.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya vifungu vyengine vya Sheria hii mtu yeyote ambaye anahisi hakutendewa haki anaweza kuwasilisha malalamiko kwa kamati ya maadili na nidhamu dhidi ya Wakili au Vakili.

(2) Mara baada ya kupokea malalamiko, katibu wa kamati ya maadili na nidhamu atawasilisha malalamiko hayo kwa kamati ya maadili na nidhamu haraka iwezekanavyo.

Uwezo wa kamati ya maadili na nidhamu.

48.-(1) Kamati ya maadili na nidhamu baada ya kuzisikiliza pande zote mbili inaweza, kuamuru kufutwa kwa malalamiko, au kama kamati imejiridhisha kuwa madai yamethibitika dhidi ya upande mwengine kamati ya maadili na nidhamu inaweza:

(a) kumuonya muhusika;

(b) kumsimamisha muhusika kufanya kazi za uwakili au Vakili kwa muda maalum usiozidi miaka miwili.

(c) kutolewa jina la muhusika katika orodha.

(d) muhusika kulipa fidia kama itakavyoamuliwa na kamati ya maadili na nidhamu kwa mtu yeyote ambaye hakuridhika na kosa alilofanyiwa lililolalamikiwa; au

(e) kuunganishwa amri zilizotolewa na kamati ya maadili na nidhamu kama itakavyoona inafaa

(2) Amri yoyote itakayotolewa na kamati ya maadili na nidhamu chini ya masharti ya kifungu hichi kuhusiana malipo ya fidia yataandaliwa na kamati ya maadili na nidhamu na yatatekelezwa kama kwamba ni amri iliyotolewa na mahakama.

(3) Endapo ikitokezea haja ya kufidiwa katika jambo jengine litakalojitokeza baadae linalolingana na shauri liliopo, Mahakama wakati wa kufanya maamuzi katika shauri la madai itazingatia kiwango kinachobidi kulipwa kwa mujibu wa amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1)(d) cha kifungu hiki.

Taarifa na hatua kuhusiana na malalamiko.

49.-(1) Itakapofika muda wa kumalizia kusikizwa lalamiko, iwapo kamati ya maadili na nidhamu haijaliondosha shauri, Kamati ya Maadili na Nidhamu itaelezea waliyofikia, na amri waliyotoa au walizozitoa kwa mfumo wa ripoti na kuipeleka Mahakamani.

(2) Ripoti iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itawasilishwa kwa Mrajis pamoja na kumbukumbu za ushahidi zilizochukuliwa na kila waraka wa ushahidi.

(3) Mrajis atatoa kwa mlalamikaji na mlalamikiwa indhari ya kuwasilisha taarifa itakayoweza kukaguliwa na mlalamikaji, muhusika na mawakili kama wapo, lakini hazitowekwa wazi kwa umma kukaguliwa.

Taarifa na amri zilizotolewa na Kamati ya Maadili kupokelewa kama ushahidi.

50.–(1) Taarifa na amri zilizotolewa na Kamati ya Maadili na nidhamu chini ya Sheria hii zitasainiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu.

(2) Waraka wowote unaokusudiwa kua ni ripoti au ni amri uliyosainiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hichi, utapokelewa kama ushahidi katika mahakama, au katika mwenendo wowote chini ya Sheria hii na itachukuliwa kuwa ni ripoti au amri halisi bila ya kuhitaji uthibitisho mwengine wa ziada kuthibitisha yaliyomo isipokuwa kama kutaonyesha utofauti.

Ombi la mapitio.

51. Upande wowote ambao haukuridhika na amri ya kamati ya maadili na nidhamu iliyotolewa chini ya kifungu cha 48 unaweza, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea indhari iliyotolewa chini ya kifungu cha 49 (3) kupeleka maombi Mahakamani ifanye mapitio.

Kuwakilishwa katika mahakama.

52. Upande unaohusiana na madai unaweza kuwakilishwa na Wakili mbele ya Mahakama Kuu, na Kamati ya Maadili na Nidhamu itakua na haki ya kuwepo mbele ya Mahakama yenyewe au Wakili kwa ajili ya kuwasilisha Mahakam Kuu yaliyofikiwa na Kamati ya Maadili na Nidhamu kama ilivyo katika ripoti.

Kurejeshwa katika orodha.

53. Iwapo amri ya kamati ya maadili na nidhamu imetupwa katika mapitio ya mahakama , mahakam kuu inaweza kumuamuru mrajis kulirejesha jina la wakili au vakil ambaye jina lake liliondoshwa katika orodha au kufuta amri yoyote ya kumsitisha wakili au vakil kufanya kazi zake.

Kuvunja maadili ya kitaaluma.

54.-(1) Wakili au Vakili anaweza kuwa amevunja maadili ya kitaaluma ikiwa:

(a) anachukua katika kesi yoyote maelezo kutoka kwa mtu asiyekuwa amewekwa na wakili au vakil kwa niaba ya muhusika, au kutoka kwa mtu mwengine asiyetambulika kuwa ni wakala anayetambuliwa na muhusika, au mtu asiyekuwa mtumishi;

(b) amepatikana na kosa la kudanganya au vitendo visivyokubalika katika kutekeleza majukumu yake kitaaluma au ameipotosha Mahakama au amechangia Mahakama kupotoshwa hivyo kuipelekea Mahakama kutoa amri ambayo anajua kuwa siyo sahihi au isiyokubalika.

(c) kufanya makubaliano, kutoa ridhaa ya kuzuia malipo yaliyolipwa au yangelipwa kwa ajili ya huduma zake yanayotosheleza kwa matumizi au kumuezesha manunuzi kwa kazi za kisheria yeye mwenyewe au wakili mwengine au vakili.

(d) moja kwa moja au vyenginevyo, amejaribu kujitafutia kazi kama wakili au vakil kwa kumlipa mtu mwengine ambaye tayari alikwishalipwa, au ameshakubaliana au kuahidiwa kulipwa kwa kazi hiyo.

(e) anaruhusu jina lake na sifa zake kama ni wakili au vakili kutumiwa na watu wasio waaminifu.

(f) au vyenginevyo ni mkosa wa makosa yasiyo ya maadili ya kitaaluma.

(g) anaruhusu jina lake na sifa yake yoyote kama wakili au vakili kutumika kwa matangazo au utambuzi. au

(h) amevunja au ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii au miongozo iliyowekwa kwa Sheria hii.

Uwezo wa kusitisha.

55.–(1) Jaji Mkuu anaweza kumsitisha wakili au vakil kwa kukiuka maadili na anaweza kulipeleka jambo hilo kwa kamati ya maadili na nidhamu.

(2) Jaji Mkuu anaweza kuondosha amri ya kusitisha chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki wakati wowote.

(3) Usitishwaji chini ya kifungu hichi hautazidi kipindi cha miezi sita.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

Wakili na Vakili kua ni afisa wa mahakama.

56. Mtu yeyote ambaye amekubaliwa rasmi kua Wakili au Vakili atakua ni Afisa wa Mahakama na atakua anawajibika chini ya mamlaka hiyo.

Kutambuliwa.

57.-(1) Wakili atatambuliwa baina yake na wengine kwa mujibu wa tarehe aliposaini orodha.

(2) Mwanasheria Mkuu, wakili wa Serikali, au wakili aliyeteuliwa kuwakilisha Serikali kwa nafasi yoyote itapaswa kuanza kutambuliwa pale ambapo yupo na mawakili wengine.

(3) Mavakili watatambuliwa baada ya mawakili na kati yao wenyewe kwa mujibu wa utangulizi.

Kuridhiwa kwa waraka.

58.-(1) Waraka wowote ulioandikwa au kutayarishwa na wakili au vakili utaridhiwa kwa kuwekwa jina la wakili au vakili ambaye ameuandaa au kuutayarisha waraka huo.

(2) Kifungu hiki hakitatumika kwa;

(a) afisa yeyote wa umma anaetumikia Serikali kuandaa au kutayarisha waraka katiak kutekeleza majukumu yake; na

(b) Mtu yeyote alieajiriwa kwa kuikamilisha au kutoa kivuli cha ya waraka wowote.

Ombi kuambatishwa na hati ya kiapo .

59. Ombi litakalofanywa chini ya sheria hii litaambatishwa na hati ya kiapo.

Mamlaka ya kundesha kesi.

60. Isipokua kama itaelezwa vyenginevyo katika sheria hi,i makossa yote chini ya sheria hii yataendeshwa na mahakama za mkoa .

Adhabu za jumla.

61. Mtu atakayekwenda kinyume na masharti sheria hii ambapo adhabu yake haikkuwekwa adhabu atakua ametanya kosa na atakapotiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopungua shilling laki sita au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote viwili

Makubaliano yanayomu-ondosha wakili au vakil katika mzembe kutokuku-balika.

62. Sharti lolote katika Makubaliano yoyote kwa wakili au vakil ambayo mtaka huduma anamtoa wakili au vakil jukumu la uzembe au kumuondosha wajibu wa kutekeleza jukumu halikubaliki.

Miongozo inayotolewa na Jaji Mkuu.

63.-(1) Jaji Mkuu anaweza kuweka miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jaji mkuu anaweza kuweka miongozo kuhusiana na:

(a) mavazi stahiki ,au , vishali kwa mawakili au vakil kwa ajili ya kusimama mbele ya mahakama;

(b) kulinda maslahi au mali ya mtaka huduma wa wakili au vakil ambaye:

(i) jina lake limeondolewa katika orodha;

(ii) haki ya kufanya kazi imesitishwa; au

(iii) kwa sababu nyengine yeyote hawezi kufanya kazi za kisheria;

(c) Masharti na taratibu kuhusiana namaombi ya cheti cha ruhusa ya kufanya kazi za kisheria na cheti kwa Mkuu wa viapo.

(d) Ufafanuzi wa ada

(e) Malipo ya wakili na vakili;na

(f) kutunza hesabu ya benki kwa Wakili au Vakili.

Kufuta na kubakiza.

64.-(1) Sheria zifuatazo zinafutwa :

(a) Sheria ya Mawakili Sura ya 28 ya 1941; na

(b) Sheria ya Wakuu Wa Viapo Sura ya 29 ya 1948.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa sheria zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hichi, wakili anayefanya kazi za uwakili au Mkuu wa viapo ambaye amekubaliwa na kupewa ruhusa ya kufanya kazi kabla kuanza kutumika kwa Sheria hii itachukuliwa kwamba amekubalika rasmi na kupewa ruhusa ya kufanya chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Cheti au waraka wowote uliyotolewa chini ya sheria iliyofutwa itachukuliwa kuwa umetolewa kwa mujibu wa masharti yaliyo sawa yaliyomo katika sheria hii.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Mawakili Sura ya 28 ya 1941 na Sheria ya Wakuu Wa Viapo Sura ya 29 ya 1948 na kutunga Sheria mpya ya mawakili ya Zanzibar itakayoongoza na kusimamia mambo yanayohusiana na watendaji wa sheria wakiwemo mawakili, mavakil na wakuu wa viapo Mawakili na kuwa na jukumu, pamoja na mambo mengine la kusimamia usajili wa watu wanaokubaliwa kuwa mawakili vakili naWakuu wa viapo Zanzibar,pia kuweka vigezo kwa mtu anayetaka kuwa katika hao pamoja na kuhakikisha kuwa mawakili wote na mavakili pamoja na wakuu wa viapo wanaofanya kazi za Sheria au kutoa huduma za kisheria zanzibar wanakidhi vigezo kitaaluma, maadili ya kitaaluma na mienendo yao iwe yenye kukubalika kutokana na huduma za Kisheria wanazotoa kwa kuhakikisha maslahi na upatikanaji haki kwa zanzibar vinalindwa ipasavyo.

Mswada huu umegawika katika Sehemu kuu Nane:

Sehemu ya kwanza: imeanzia kifungu cha 1 hadi cha 3 ambavyo vinajumuisha Jina fupi na kuanzakutumika,Matumizi,naUfafanuziwamanenoyaliyotumikakatika Mswadawa Sheria hii.

Sehemu ya Pili: imeanzia kifungu cha 4 hadi cha 13 ambavyo vinajumuisha Kuanzishwa na muundo wa Baraza la Mawakili, Muda wa mwenyekiti kushikilia nafasi yake, Kazi za Baraza la Mawakili, Uwezo wa Baraza la Mawakili, Ukomo wa nafasi ya mwenyekiti, Uwezo wa Baraza la Mawakili, Vikao vya Baraza la Mawakili, Akidi, Utaratibu wa kuendesha vikao na Matumizi ya Baraza la Mawakili.

Sehemu ya Tatu: imeanzia kifungu cha 14 hadi 25 ambavyo vinajumuisha Maombi ya kukubaliwa kuwa Wakili, Maombi ya kukubaliwa kuwa Vakili, Maombi ya ruhusa kwa Wakili wa kigeni kusimamia kesi, Jaji mkuu kuhamishia maombi kwa Baraza la Mawakili, Baraza la Mawakili, Kuruhusiwa kuwa Wakili au Vakili, Ruhusa inayotolewa kwa Wakili wa kigeni, Orodha, Jukumu la Mrajis, Haki za wakili na Vakili, Mamlaka ya kufanya kazi za kiheria na Kuondoshwa.

Sehemu ya Nne: imeanzia kifungu cha 26 hadi 28 ambavyo vinajumuisha Cheti cha ruhusa ya kufanya kazi, Kukataliwa cheti cha kufanya kazi na Hesabu za mtaka huduma.

Sehemu ya Tano: imeanzia kifungu cha 29 hadi 35 ambavyo vinajumuisha Kuanzishwa kwa kamati ya ushauri wa malipo, Kazi za kamati ya ushauri wa malipo,

Sehemu ya Sita: imeanzia kifungu cha 36 hadi 40 ambavyo vinajumuisha Kukubaliwa kwa wakuu wa viapo, Kuingizwa katika orodha na kupewa cheti cha Mkuu wa Viapo, Azabu kwa kufanya kazi kinyume na Sheria, Katika ithibati ya kiapo kuanishwa pahala na tarehe na Jaji au Hakimu wa Mkoa kuwa na baadhi ya uwezo wa Mkuu wa Viapo.

Sehemu ya Saba: imeanzia kifungu cha 41 hadi 55 ambavyo vinajumuisha Kamati ya maadili na nidhamu, Vikao vya Kamati ya Maadili na Nidhamu, Akidi, Taratibu za kikao, Matumizi yatakayofanywa na kamati ya maadili na nidhamu, Kubakiza uwezo wa Mahakama katika hatua ya kinidhamu, Malalamiko dhidi ya Wakili au Vakil, Uwezo wa Kamati ya maadili na nidhamu, Taarifa na hatua kuhusiana na malalamiko na Uwezo wa kusitisha.

Sehemuya Nane: ambayo ni ya mwisho kuanzia kifungu cha 56 hadi 64 ambavyo vinajumuisha: Wakili na Vakili kua ni Afisa wa Mahakama, Kutambuliwa, Kuridhiwa kwa waraka, Ombi kuambatanishwa na hati ya kiapo, Mamlaka ya kuendesha kesi, Adhabu za jumla, Makubaliano yanayomuondosha Wakili au Vakili katika uzembe kutokukubalika, Miongozo inayotolewa na Jaji Mkuu na Kufuta na kubakiza.

ZANZIBAR
06 Novemba, 2019

(KHAMIS JUMA MWALIM)
WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA
ZANZIBAR

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI ZANZIBAR - 2019